# Wafanyabiashara wapigia chapuo Tanesco kugawanywa




Makao makuu ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco). Wadau wa biashara wanapendekeza shirika hilo kufumuliwa ili kuongeza tija ya upatikanaji wa nishati ya umeme nchini. **Picha na Maktaba**

**SAUTI ZA WATU**

**Faus Duma, Iringa**

Kuhusu lumbesa; nashauri yajengwe maghala ya kutosha ili wakulima wahifadhi mazao yao, wasiuzie shambani. Mbili, mazao yauzwe kwa kilo na siyo kwenye madebe au plastiki, tatu, itengenezwe mifuko yenye vipimo halali na siyo viroba. Nne, mazao yanapoingia sokoni yakaguliwe ujazo wake. Tano, kuwapo na bei maalumu kwa kila zao na izingatiwe.

**Julius Martin**

Kabla ya kutunga sheria ndogo za halmashauri ni vizuri wadau wakashirikishwa kupitia taasisi husika kama TCCIA. Kwa mfano mimi nina nyumba ya wageni ninatakiwa kulipa kodi ya mapato, tozo ya hoteli ya asilimia 20 ya mapato kabla ya kutoa matumizi, ada ya bango, hii haijalishi kama una bango au huna. Pia, nadaiwa kifaa cha kuzima moto, hii ununua mwenyewe mitungi na kuihudumia kwa gharama zako, ada ya leseni. Hivi vyote ni kodi kwa mfanyabiashara mmoja. Usitarajie maendeleo hapo.

(Kwa maoni kuhusu mazingira ya kibiashara Tanzania tuma ujumbe kwenda 0786240172. Ujumbe utakaochapishwa utazawadiwa Sh30,000 za muda wa maongezi).

Wadau wa biashara nchini wanaiona hatua ya Serikali kutaka kuligawa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kama hatua muhimu katika kuongeza ufanisi wa kushughulikia matatizo ya nishati ya umeme nchini.

Hivi karibuni, kijarida cha mtandaoni cha Tanzania Invest kinachochapishwa kila wiki, kiliandika kuwa, Serikali imebaini kampuni binafsi sita zitakazochukua nafasi ya Tanesco katika kuzalisha na kusafirisha umeme ifikapo mwaka 2022.

Hatua hiyo inalenga kuisaidia Tanesco katika utafutaji wa fedha za miradi ya umeme, pamoja na kupunguza gharama za nishati hiyo.

Kampuni hizo sita zitakuwa katika nikoa ya Mashariki, Kaskazini-Mashariki, Kaskazini-Magharibi, kati, Kusini Mashariki na nyanda za juu kusini ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme nchi nzima na hivyo kuchochea maendeleo.

Kuwepo kwa kampuni hizo sita ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa kuigawa Tanesco katika sehemu tatu; uzalishaji, usafirishaji na usambazaji ili kuondokana na mfumo wa sasa ambako shirika hilo linafanya kazi hizo zote.

Mpango huu pia uko sambamba na mkakati wa maboresho ya sekta ya umeme 2014-2025 yanayofanywa na Wizara ya Nishati na Madini, ambayo yanalenga kushirikisha sekta binafsi katika kuzalisha umeme pamoja na kuboresha uwezo wa kiutendaji na kifedha wa Tanesco.

Katika mkakati huo, Tanzania inatarajia kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka takriban megawati 1,500 za sasa hadi kufikia megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025.

''Hata hivyo, Serikali haiwezi kufanya uwekezaji huo peke yake na sasa inapitia muundo wa Tanesco na kuhakikisha inamaliza madeni yake ifikapo mwaka 2021 na ugatuzi wake unatarajiwa kukamilika,'' kilisema kijarida hicho kikimnukuu kamishna wa nishati na mambo ya mafuta, Hosea Mbise.

**Wafanyabiashara wapigia chapuo**

Shirikisho la Viwanda (CTI) pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), wamepongeza hatua ya ugawaji wa Tanesco na kuiita mwelekeo mzuri katika kushughulika changamoto za umeme.

"Huu ni mwelekeo mzuri ukizingatia kwamba tumekuwa tukipigia kelele suala la kuigawa Tanesco kwa muda mrefu sasa. Ikumbukwe kamba Tanzania inalenga kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025 na hii ina maana kwamba hata mahitaji ya umeme yatakuwa makubwa zaidi,'' anasema Mwenyekiti wa CTI, Dk Samuel Nyantahe.

Anasema mpango huu pia unaenda sambamba na ushirikiano kati ya sekta binafsi na ile ya umma (PPP) na kwamba juhudi za Serikali katika kuongeza umeme zinapaswa kuungwa mkono.

Dk Nyantahe anaeleza kwamba matumizi ya gesi katika kuzalisha umeme yameongeza upatikanaji wa nishati, lakini changamoto za umeme bado zipo.

Mkurugenzi mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye anasema kuigawa Tanesco ni kilio cha muda mrefu kutoka sekta binafsi na kwamba itaongeza ufanisi katika sekta ya nishati.

Hata hivyo, anaitaka Serikali kuandaa mazingira mazuri, kwa ajili ya sekta hiyo binafsi kushiriki katika kuzalisha umeme.

"Changamoto kubwa ipo katika kupanga bei. Serikali mara nyingi hupanga bei yake itakayonunua umeme kutoka kwa mwekezaji binafsi, ambayo haizingatii gharama za uzalishaji. Hii inawafanya wawekezaji wengi wawe na hofu," anasema.

Anasema kwamba umeme unaopotea kutokana na kukosekana kwa ufanisi unafikia karibu asilimia 40, na kwamba kuigawa Tanesco huenda kukasababisha hata gharama za umeme kushuka.

Kumekuwepo mapendekezo ya muda mrefu ya kubadili muundo wa Tanesco ili ibaki na kazi ya kusafirisha umeme na kutenganisha usafirishaji na usambazaji. Hatua hii ililenga kuongeza ushindani katika uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Hata hivyo, Serikali imeendelea kuikumbatia Tanesco kwa sababu ambazo wadau wanasema haziko wazi.

CTI pia ilipendekeza hivyo katika utafiti wake wa kisera wa mwaka 2011 ambao uliwasilishwa kwa wadau.

Kukatika umeme mara kwa mara, kuchelewa kutoa bili za wateja, kuchelewa kushughulikia matatizo ya wateja, kuchelewa kuunganisha wateja wapya wa umeme, ni baadhi ya dosari zilizobainishwa katika utafiti huo.

Kukosekana kwa umeme wa uhakika kunatajwa kama mojawapo ya vikwazo vikubwa vya uwekezaji nchini Tanzania, kwa kuwa wawekezaji hutilia maanani kuhusu nishati hii.

***Kwa maoni kuhusu mazingira ya kibiashara Tanzania tuma ujumbe kwenda 0786240172. Ujumbe utakaochapishwa utazawadiwa Sh30,000 za muda wa maongezi)***

**UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA**

BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo